SUCCESS BUILDERS

# MAUNGAMO 31 YA MJENZI MFANISI- Mel Mullen

**#1. Mungu ana Mipango mizuri kwangu.**

Yeremiya 29:11 “kwa maana ninajua mipango niliyo nayo kwa ajili yenu,’’ asema BWANA. “Ni mipango ya kuwafanikisha na wala si ya kuwadhuru, ni mipango ya kuwapa tumaini katika siku zijazo.

**#2. Maisha yangu ya baadaye ni makuu.**

Mwanzo 12:2 “Mimi nitakufanya taifa kubwa na nitakubariki, Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka.

**#3. Niko yule Mungu anasema Niko.**

Warumi 8:16 “Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu ya kwamba sisi tu watoto wa Mungu.”

**#4. Mimi ni mwenye haki.**

2 Wakorinto 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

**#5. Nina mamlaka. Ninachukua Utawala.**

Mwanzo 1:28 “Mungu akawabariki na akawaambia, “Zaeni na mkaongezeke, mkaijaze tena dunia na kuitiisha. Mkatawale samaki wa baharini, ndege wa angani na kila kiumbe hai kiendacho juu ya ardhi.’’

**#6. Uongozi ni njia ya maisha yangu.**

KUMBUKUMBU LA TORATI 28:13 « BWANA atakufanya kichwa, wala si mkia. Kama utazingatia maagizo ya BWANA Mungu wako ninayokupa siku hii ya leo na kuzifuata kwa bidii, daima utakuwa juu, kamwe hutakuwa chini.

**#7. Namiliki Mbingu na Dunia.**

Mwanzo 14:19 “Akambariki Abramu, akisema, “Abarikiwe Abramu na Mungu Aliye Juu Sana, Muumba wa mbingu na nchi.

**#8. Nachukua hatua za Imani - Ninafanikiwa**

Yoshua 1:3 “Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga nimewapa, kama vile nilivyomwahidi Mose. Zaburi 1:3 “Mtu huyo ni kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao huzaa matunda yake kwa majira na majani yake hayanyauki. Kila afanyalo hufanikiwa.

**#9. Nina ujasiri pasipo uoga**

WAAMUZI 6:12 “Malaika wa BWANA alipomtokea Gideoni, akamwambia, “BWANA yu pamoja nawe, Ewe shujaa mwenye nguvu.”

**#10. Mimi sina uoga**

2Timotheo 1:6,7 “Kwa sababu hii nakukumbusha uchochee ile karama ya Mungu, iliyowekwa ndani yako nilipokuwekea mikono yangu. **7**Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi.

**#11. Ujasiri -Uweza - Utiifu - Ufanisi.**

Yoshua 1:6,7 “Uwe hodari na moyo wa ushujaa, kwa sababu wewe ndiwe utakayewaongoza watu hawa kuirithi nchi niliyowaapia baba zao kuwapa. Uwe hodari tu na ushujaa mwingi. Uwe na bidii kutii sheria zote alizokupa Mose mtumishi wangu, usiziache kwa kugeuka kuelekea kuume au kushoto, ili upate kufanikiwa po pote uendako”.

**#12. Ninaweza, Ndiyo Ninaweza, Mungu amesema ninaweza.**

Wafilipi 4:13 “Naweza kuyafanya mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu”.

**#13. Mimi ninaweza**

Hesabu 13:30 “Kisha Kalebu akawanyamazisha watu mbele ya Mose na kusema, “Imetupasa kupanda na kuimiliki nchi, kwa maana hakika tunaweza kufanya hivyo.”

**#14. Majitu ni Mkate wangu wa kila siku.**

Hesabu 14:8-10 “ **8**Ikiwa BWANA anapendezwa nasi, atatuongoza kuingia katika nchi ile, nchi itiririkayo maziwa na asali, naye atatupa nchi hiyo. **9**Ila tu msimwasi BWANA. Wala msiwaogope watu wa nchi hiyo, kwa sababu tutawameza. Ulinzi wao umeondoka, lakini BWANA yupo pamoja nasi. Msiwaogope.’’ **10**Lakini kusanyiko lote likazungumza juu ya kuwapiga kwa mawe. Ndipo utukufu wa BWANA ukaonekana katika Hema la Mkutano kwa Waisreali wote”.

**#15. Nakiombea, Nakitaja, Nakipata.**

MARIKO 11:23 “Amin, amin nawaambia, mtu ye yote atakayeuambia mlima huu ‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ wala asione shaka moyoni mwake, bali aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. ”

**#16. Mipango - Njia - Imeongozwa na Bwana.**

**MITHALI** 3:5 “Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe”.

**#17. "Ndiyo" ni sehemu yangu**

Matendo ya Mitume 16:6-10 “Paulo pamoja na wenzake wakasafiri sehemu za Firigia na Galatia, wakiwa wamekatazwa na Roho Mtakatifu wasihubiri neno huko Asia. **7**Walipofika kwenye mpaka wa Misia, wakajaribu kuingia Bithinia lakini Roho wa Yesu hakuwaruhusu. **8**Kwa hiyo wakapita Misia, wakafika Troa. **9**Wakati wa usiku Paulo akaona maono, mtu wa Makedonia amesimama akimsihi, “Vuka uje huku Makedonia ukatusaidie.” **10**Baada ya Paulo kuona maono haya, mara tulijiandaa kuondoka kwenda Makedonia tukiwa tumesadiki kwa sababu tuliona kwa hakika kwamba Mungu ametuita kuhubiri habari njema huko.

**#18. Mungu yu pamoja nami.**

Kutoka 33:14 “BWANA akajibu, “Uso wangu utakwenda pamoja nawe, **nami nitakupa raha.’’**

**#19. Ninaishi katika kibali cha Mungu.**

Zaburi 30:5 “Kwa maana hasira yake ni ya muda mfupi, bali upendo wake hudumu siku zote, inawezekana kilio kikawepo usiku kucha, lakini asubuhi kukawa na furaha”.

**#20. Kwa Kila shida napokea mara dufu.**

Ayubu 42:12 “BWANA akaibariki sehemu ya mwisho ya maisha ya Ayubu kuliko ya kwanza. Alikuwa na kondoo 14,000, ngamia 6,000, jozi za mafahali 1,000 na punda wa kike 1,000”.

**#21. Nina Furaha Katika Kila jaribu.**

Yakobo 1:2 “Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu mnapopatwa na majaribu mbalimbali”.

**#22. Uvumilivu hunifanya mtu mkamilifu.**

Yakobo 1:3 “kwa sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi timilifu, ili mpate kuwa wakamilifu, mmekamilishwa, bila kupungukiwa na kitu cho chote.”

**#23. Mbingu zimefunguka na nimebarikiwa!Barikiwa...Barikiwa.**

Malaki 3:10 “Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu. Nijaribuni katika hili,’’ asema BWANA Mwenye Nguvu, ‘’nanyi mwone kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka nyingi mpaka mkose nafasi ya kutosha au la.”

**#24. Mungu ndiye mpaji wangu.**

Wafilipi 4:19 “Naye Mungu wangu atawajaza ninyi kila mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri Wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.

**#25. Mimi nitaishi katika nchi ya "zaidi ya kutosha".**

Hesabu 14:8 “Ikiwa BWANA anapendezwa nasi, atatuongoza kuingia katika nchi ile, nchi itiririkayo maziwa na asali, naye atatupa nchi hiyo.

**#26. Mavuno yangu yaja.**

Wagalatiya 6:7-9 “Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna. Apandaye kwa mwili, katika mwili wake, atavuna uharibifu, lakini yeye apandaye katika Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. **9**Hivyo, tusichoke katika kutenda mema, kwa kuwa tutavuna kwa wakati wake tusipokata tamaa.

**#27. Ninaongeza tabia nzuri. Sitaanguka kamwe.**

2Petro 1:3-10 “ **3**Uweza Wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake mwenyewe…….. hamtajikwaa kamwe”.

**#28. Nina Afya ya kiungu.**

1 Petro 2:24 “Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba,tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa.

3 Yohana 2: “Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako kama vile roho yako ifanikiwavyo.”

**#29. Ninaishi maisha pasipo kipimo.**

Marko 10:27 “Yesu akawatazama, akawaambia, “Kwa mwanadamu hili haliwezekani, lakini kwa Mungu sivyo. Yote kwa Mungu yanawezekana.’’

**#30. Nimelindwa** Zaburi 91:10 “basi hakuna madhara yatakayokupata wewe, wala maafa hayataikaribia hema yako.

**#31. Mungu huanza- Mungu humaliza**

Wafilipi 1:6nina hakika kwamba, Yeye aliyeianza kazi njema mioyoni mwenu, ataiendeleza na kuikamilisha hata siku ya Kristo Yesu.”

**Mungu anaweza - Fikiri - Uliza – Tenda – Tarajia [Waefeso 3:19-20]**